**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA (W) RORYA**
**SHULE YA SEKONDARI BUTURI**
**S.L.P 47**
**RORYA.**


**Namba za Simu…………………..**

**Mkuu wa Shule 0759 447333**

**Makamu Mkuu wa Shule0756867542/0752523598**

**Matron/Patron0766744810/0743673474**

**Shule ya Sekondari BUTURI**

**S.L.P.47 RORYA/TARIME**


**Tarehe 02/05/2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUTURI HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA MKOA WA MARA MWAKA ..............**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka............... na atasoma tahasusi ya ………….

**2.** Shule ya Sekondari Buturi ipo Wilaya ya Rorya Mkoa wa Mara. Kwa watakaotoka Mwanza wapande mabasi yanayoenda **Tarime** ambayo yanapatikana katika stendi ya **NYAMONGOLO Mwanza** washuke **Oliyo,** umbali kidogo tu kutoka **daraja la Mto Mara.** Kisha wapande pikipiki kutoka **Oliyo** hadi Buturi Sekondari kwa gharama ya Tsh. 4,000/= tu.

Kwa watakaotoka Musoma wapande magari ya **TARIME** kwa gharama ya **Tsh 5,000** washuke **OLIYO** kisha wachukue pikipiki mpaka Buturi sekondari kwa gharama ya Tsh 4,000.

Kwa wanaotokea Tarime wapande haisi au mabasi yanayoelekea Musoma na washuke **Oliyo,** kisha wapande pikipiki hadi Buturi Sekondari kwa gharama **ya Tsh. 4,000**/=tu. Pia kuna usafiri wa haisi wa moja kwa moja kutoka tarime hadi Buturi Sekondari ambao unapatikana nyakati za saa 4 hadi saa 5 asubuhi kwa **Tsh. 5,000/=**

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **...............** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe  Mwisho w………… kuripoti ni tarehe **………………**

## 3. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 3.1 Sare za Shule

1. Suruali mbili (02), moja **DARK BLUE NA KHAKI**.Suruali zisiwe za modo,suruali ziwe na marinda 2 na yenye mfuko mmoja nyuma na mifuko miwili pembeni.Suruali chini iwe na mpindo(turnup). Pia aje na suruali nyeusi ya kitambaa kwa ajili ya kushindia.

   Zingatia: Mwanafunzi asishone suruali zenye mfumo wa model.

2. Shati mbili (02) au zaidi nyeupe za MIKONO MIREFU na zenye mfuko mmoja tu, aje nazo (Shati daima itachomekwa ndani ya suruali ivaliwapo, kadhalika na T-shirt.
3. T-shirt mbili (02) zinapatikana shule kwa gharama ya Tsh 24,000/=
4. Aje na Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba jozi mbili (02) visiwe na visigino virefu na muundo wa ‘boot’, .
5. Aje na Soksi nyeusi jozi nne (04) na zisiwe na mistari au madoadoa .
6. Sweta moja ya kuvaa (Special) wakati wa baridi **Tsh 20,000/=** Aje na pesa hiyo
7. Mkanda mweusi wa kiuno (Upana inchi 1.5) kufungia suruali
8. Aje na Viatu vya raba vya michezo na shughuli za nje pia aje na Tshirt na bukta yake rangi bluu na nyeusi(aina ya jezi)
9. Aje na Track suit nyeusi au blue.
10. Viatu vya wazi (Open Shoes) vitavaliwa baada ya vipindi vya darasani.
11. Koti la maabara jeupe – litavaliwa wakati wa mafunzo kwa Vitendo (Practicals). Kwa wanafunzi wa sayansi tu. (CBG na PCB)

**NB; Mwanafunzi hatakiwi kuja na mavazi au vitu vingine ambavyo havijaelekezwa katika form hii.**

### 3.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

1. Godoro la ‘Sponge’ la upana wa futi 2.5 x 6 aje nayo.
2. Shuka mbili (02) rangi ya blue bahari (light blue) na pinki aje nazo.
3. Ndara/Kanda mbili aje nazo.
4. Sanduku la bati na kufuli kwa ajili ya kutunza vitu vyake (ni lazima) aje nayo.
5. Chandarua rangi ya bluu, aje nacho.
6. Ndoo ya kuchotea maji ya lita ishirini (20) aje nayo.
7. Ndoo ndogo ya kuogea ya lita kumi (10).
8. Aje na Taulo
9. Aje na dumu la lita tano la kutunzia maji ya kunywa
10. Toilet paper tano kwa ajili ya matumizi yake aje nazo zitakaguliwa.
11. Sahani, bakuli, kijiko na kikombe cha nusu lita, aje navyo.
12. D-light ndogo ya **Solar** ya kutumia umeme ukikatika.
13. Pia usisahau kumpa mwanao fedha za kutoshakwa ajili ya matumizi yake binafsi.
14. Blanketi kwa ajili ya kujifunika wakati wa baridi.
15. Ream mbili za karatasi za photocopy (Double A4) kwa muhula au NNE kwa mwaka.

16. Madaftari makubwa CounterBooks Quire 3, au Quire 4 yasiyopungua saba (7) na pia daftari ndogo ya mazoezi yasiopungua (07).
17. Flat file moja.
18. Graph Pad 02.
19. Mathematical set.
20. Scientific Calculator (kwa wanaosoma masomo ya sayansi) aje nayo.
21. Dissecting kit (kwa wanaosoma masomo ya sayansi)
22. Dawa ya chooni lita tano (05)
23. Jembe lenye mpini 01, Reki 01, mfagio laini 01, mfagio mgumu 01, chelewa 01, mopa 1au sequezer 1 na fyekeo 1.

**3.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Malipo yote yafanyike kwenye akaunti ya shule NO 30401200129-NMB BUTURI SEC SCHOOL. ISIPOKUWA FEDHA YA NEMBO NA KITAMBULISHO ILETWE MKONONI**

**NB:Mwanafunzi aje na bima ya afya kwa ajili ya matibabu yake.(endapo mwanafunzi atalazimika kupata matibabu tofauti na kituo jirani(zahanati),mzazi utahusika kwenye gharama za usafiri)**

## 4. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka **1978** na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka **1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 4.1 Sheria na Kanuni za Shule

**Sheria na kanuni hizi huzingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII NA TABIA NJEMA. Hivyo wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri Kwa heshima na tabia pia kauli vitendo kwa sababu lengo la elimu ni kuwajenga katika hayo. Kwahiyo ni lazima wazingatie mambo yafuatayo;**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.; hivyo mwanafunzi atasimama pale anapomsalimia Mwalimu,mtumishi wa shule au yeyote anayemzidi umri.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; hivyo haruhusiwi kufuga ndevu, nywele,kunyoa kipara wala kiduku, kutia dawa nywele wala kujichubua ngozi, kuvaa mapambo mfano heleni bangili na vitu vya kiimani kama rozali, kofia,kanzu, vilemba wala suruali fupi kwa kuwa shule siyo ya dini bali ya SERIKALI. Badala yake miongozo ya kuendesha shughuli za kidini atapewa shuleni na uongozi au walimu walezi.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Mwanafunzi ahudhurie paredi na wito wa uhakiki na uwepo wake shuleni muda wowote akihitajika.
xi. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha ofisi ya makamu Mkuu wa shule kila baada ya likizo au ruhusa maalumu.
xii. Mwanafunzi asipige kelele,yowe au vitendo vyovyote vya kiusumbufu na vyenye kuzua taharuki anapokuwa eneo la shule muda wote.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi. Hivyo asije na simu kabisa kwani atarudishwa shuleni siku hiyo hiyo.**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**4.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xix. Kutoroka shuleni au kwenda nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya uongozi wa shule

**5. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**6.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**




**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- ➢ **Mkuu wa shule 0714945311**
- ➢ **Makamu Mkuu wa Shule 0756867542/0752523598**
- ➢ **Mwandamizi Taaluma 0713518737**
- ➢ **Mwandamizi Malezi 0762785996**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA**
**SHULE YA SEKONDARI BUTURI**
**HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la Ukoo …………………..Jina la kwanza ………..…. Jina la Kati ………………
2. Jina la Mzazi/Mlezi ………………………………...…………………...……………
3. Kama ni Mlezi: Uhusiano …………………………..….. Namba ya simu……………….
4. Anwani ya Kudumu ya Mzazi/Mlezi ……………………………….……..…………..
5. Mahali mwanafunzi alipozaliwa: Mtaa Wa/Kijiji c……………..….. Kata ya ………...….
   Wilaya ya ………………………………………….. Mkoa wa ……………………….
6. Dini ……………………………..…….. Dhehebu ……………………..……………
7. Unaingia Kidato cha …………………..……. Tarehe/Mwaka ……………..………
8. Kutoka shule ya Sekondari …………………… Wilaya ……………… Mkoa …………
9. Mzazi wako anafanya kazi ya ajira/Mkulima/Biashara ………………….Mahali ………
10. Usafiri kutoka hapa shuleni hadi nyumbani kwenu ni: (Toa Maelezo).
    (1) ………………………………………………………………………………….
    (2) …………………………………………………………………………………
    (3) ……………………………………………………………………………..……….
11. Ndugu Wengine ambao wanaweza kupelekewa habari juu yako/Maswala ya shule ni:-
    (i) ………………… uhusiano ……………. namba za simu …………………………
    (ii) ………………… uhusiano ……………. namba za simu …………………………
    (iii) ………………… uhusiano ……………. namba za simu …………………………
12. Kabla hujaja hapa shuleni umepimwa na daktari? Ndiyo/Hapana.
    Ni ugonjwa upi ni wa kudumu kwako? ……………………………………...……………
13. Sifa maalumu kama unazo/yo……………………………………..…….………………..
14. Unalipiwa/Utalipiwa Karo na: (Taja jina anwani yake na namba za simu)
    ……………………………………………………………..……………………………
15. Taarifa za Wazazi wako: Wapo
    ………………………………….………………………….
    Wamefariki ……………….……………………...…. (Weka alama ya vyema panapohusika).

Nakiri kuwa maelezo yaliopo hapo juu ni sahihi.

**…………………………………**
**SAINI YA MWANAFUNZI**

**………………………...…….**
**SAINI YA MZAZI/MLEZI**

## HATI YA KUKUBALI:

Mimi (Jina la mwanafunzi) ……………………………………… nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii. Naahidi kufuata sheria zote za shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

**Saini ya Mwanafunzi …………………………. Tarehe …………………………**

## TAMKO LA MZAZI/MLEZI:

Mimi Mzazi/Mlezi (Jina) ……………………………….. ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ……………………………..………… nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Buturi ambako Kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza Mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule. Aidha naahidi kushirikiana na Uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe Raia bora na mwema wa Taifa letu.

**Saini ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………Tarehe ………………………..**

**THE PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL ADMINISTRATIONS**
**BUTURI SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**
***(To be filled by an Authorized Government Medical Officer)***

Full name of Student ……………………………………………………….
Age ……………………..
Height (in cms) ………………………..…… Weight (in kgs)……………………………….

1. Blood count …………………….. (Red and White)………………..……..
2. Stool Examination …………………………………………………..…..
3. Urine analysis ……………………………………………………..….
4. Syphilis and other V.D …………………………………………….........
5. T.B. and Leprosy Test ……………………………………………….…
6. Eye Test ……………………………………………………..……….
7. Ear Test ………………………………………………………………
8. Chest Test …………………………………………………………..…
9. Abdominal Test …………………………………………………….....
10. Blood Group (very crucial) ……………………………………..………
11. Spleen…………………………………………………………………
12. H.I.V. Test, Positive …………………..…… Negative ……………..……...

(Tick where necessary)

Additional information e.g. Physical defects or impairment, infections, chronic or family Diseases (e.g. Sickle cell)
……………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………
I (full name) ………………………………………………… Certify that the above student is fit/is not fit pursue Secondary Education.

Designation ……………………………….

Station ………………………………Signature………………………………….

Date……………………………………... Rubber Stamp …………